# TANROADS

Jarida Maalumu

Oktoba 2022

Tanzania National Roads Agency
TANROADS
Good roads for national development

# Rais Samia aifungua barabara ya Nyakanazi- Kabingo yenye urefu wa kilometa 50



Limeandaliwa na kitengo cha Habari na Mawasiliano- TANROADS



# Wananchi wampongeza kwa kuufungua zaidi mkoa wa Kigoma

**NA LELA MUHAJI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan Oktoba 16, 2022 akiwa Wilayani Kakonko, Mkoani Kigoma amefungua rasmi barabara ya Nyakanazi- Kabingo( km.50) ikiwa imejengwa kwa takriban shilingi bilioni 43 na ujenzi wake kusimamiwa na TANROADS.

Akizungumza katika ufunguzi wa barabara hiyo , Rais Samia alisema Serikali imeamua kuifungua barabara hiyo, pamoja na kuweka mawe ya msingi, ikiwa ni juhudi za Serikali za kuleta maendeleo kwa wananchi.

" Tuko katika. ziara Mkoani Kigoma, tumeanza na wilaya ya Kakonko, Mradi wa maji Kakonko,, Hii ni ishara kubwa Serikali imeamua kuleta maendeleo" Alisema Mhe. Rais.

Aliongeza " Ufunguzi wa barabara ya Nyakanazi- Kabingo ni moja ya ahadi za Serikali kurahisisha shughuli za kibiashara kwa wananchi.

Pia uwepo wa miradi mbalimbali itasaidia kukuza maendeleo kwa wananchi na wananchi waendelee kuchapa kazi kwa bidii".

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Makame Mbarawa alisema ujenzi wa barabara hiyo ni kichocheo kikubwa cha uchumi, na kumpongeza Rais Samia kwa kazi kubwa aliyofanya hadi kukamilika kwa mradi huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakazi wa Kakonko wamepongeza juhudi za Rais Samia na Serikali anayoiongoza kwa kuufungua zaidi mkoa wa Kigoma hususan katika sekta ya ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Barabara ya Nyakanazi- Kabingo inaunganisha Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, na Mwanza na pia kuunganisha nchi jirani za Burundi kupitia mpaka wa Manyovu.

Ujenzi wa barabara hiyo ni mkakati wa Serikali kuhakikisha barabara zote zinaunganisha mikoa na nchi jirani, pamoja na zile za ndani zinajengwa kwa kiwango cha lami.



"Nia yetu ni kuifanya **Kigoma** kuwa Mkoa wa kimkakati kwa **uwekezaji na biashara**. Hilo linatimia kwanza kwa kuwa na **umeme wa uhakika** na **barabara zinazopitika** muda wote na yote serikali inafanya."

**Mhe. Samia Suluhu Hassan**
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*





# Rais Samia atangaza nia kuifanya Kigoma kuwa mkoa wa kimkakati



## Ataja kipaumbele cha Serikali kujenga barabara kuu zote kwa kiwango cha lami

**NA MWANDISHI WETU**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema nia na malengo ya serikali ya awamu ya sita ni kuufanya mkoa wa Kigoma kuwa mkoa wa kimkakati kiuwekezaji na kibiashara.

Pia, amesema azma hiyo itaifanya Kigoma kutoka mkoa wa pembezoni maskini hadi wenye utajiri mkubwa na fursa kemkem za kimaendeleo kwa wananchi na wafanyabiashara.

Rais Samia aliyasema hayo katika mkutano wa hadhara mjini Kasulu, wakati wa ufunguzi wa barabara ya Kidahwe-Kasulu yenye urefu wa kilometa yenye urefu wa kilometa 63.

**Rais Samia aliyasema hayo katika mkutano wa hadhara mjini Kasulu, wakati wa ufunguzi wa barabara ya Kidahwe-Kasulu yenye urefu wa kilometa yenye urefu wa kilometa 63. Akizungumza katika ufunguzi huo, Rais Samia alisema serikali ina dhamira kubwa na mkoa wa Kigoma ili kuharakisha maendeleo kwa wananchi na shughuli za usafirishaji kutoka sehemu moja kwenda nyingine na ndio maana inatekeleza ...**

Akizungumza katika ufunguzi huo, Rais Samia alisema serikali ina dhamira kubwa na mkoa wa Kigoma ili kuharakisha maendeleo kwa wananchi na shughuli za usafirishaji kutoka sehemu moja kwenda nyingine na ndio maana inatekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Alisema katika ziara yake ndani ya mkoa wa Kigoma, amezindua miradi mbalimbali ikiwemo ufunguzi na uwekaji wa mawe ya msingi ujenzi wa miundombinu ya barabara,





ENG. Rogatus Mativila

# Rais Samia atangaza nia kuifanya Kigoma kuwa mkoa wa kimkakati

lengo la kufanya hayo ni kuleta maendeleo kwa kasi kubwa.

Alisema kuweka mawe ya msingi na kufungua barabara mbalimbali ni kiashirio kikubwa kuwa serikali imepania kuinua uchumi wa mkoa wa Kigoma na watu wake.

"Nia yetu ni kuifanya Kigoma kuwa Mkoa wa kimkakati kwa uwekezaji na biashara. Hilo linatimia kwanza kwa kuwa na umeme wa uhakika na barabara zinazopitika muda wote na yote serikali inafanya" amesema.

Alieleza serikali inaendelea kuijenga Kigoma ili kuleta maendeleo kwa kasi kubwa na kuitoa mkoa huo kutoka mkoa wa pembeni duni na kuwa wenye uchumi imara.

Kwa mujibu wa Rais Samia, ufunguzi wa barabara hiyo iliyojengwa kwa sh. bilioni 64.7 kwa asilimia 100 ni fedha za watanzania zinazotokana na ulipaji wao wa kodi na kuwataka wafanye kazi kwa bidii.

Naye, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema mkoa wa Kigoma umekuwa ukitekelezwa miradi mbalimbali ili kuufungua mkoa huo na mikoa ya jirani na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Burundi, Rwanda na Uganda.

Alisema serikali ya awamu ya sita inatekeleza miradi mingi na hata kuwa na mipango ya kuanzisha miradi mipya, lengo ni kutimiza ahadi na maono ya serikali.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila amesema kuwa baadhi ya sehemu za Barabara ya kutoka Kidawe hadi Nyakanazi, ambayo Rais Samia ameifungua ni pamoja na Kidahwe hadi Kasulu, na sehemu ya kibondo imejengwa kwa fedha za ndani.

Mhandisi Rogatus Mativila ameyasema hayo wakati akitoa taarifa ya miradi kwa Rais Samia katika hafla za Ufunguzi wa Barabara ya KIDAHWE-KASULU( Km. 63), na uwekaji jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa barabara ya KABINGO-KIBONDO KASULU- MANYOVU ( Km. 260.6) .

Kuhusu Barabara ya Kidahwe Kasulu ambayo imekamilika na kufunguliwa na Rais Samia, Mhandisi Mativila amesema imejengwa na kampuni ya China Railway 15 Beaureau group ( CR15) kwa gharama ya shilingi Bilioni 64.7 na kusimamiwa na Mhandisi mshauri kwa gharama za shilingi Bilioni 5.7.

Kwa upande wa barabara ya Kabingo- Kasulu Mhandisi Mativila amesema Barabara hiyo inayounganisha Mikoa ya jirani kama vile Mikoa ya Kagera, Shinyanga, Geita na Mwanza na nchi jirani ya Burundi kupitia mpaka wa manyovu imekua ikipitika kwa shida kipindi cha mvua hivyo imefikia mahala inabidi ijengwe.

Hivyo, amesema ujenzi wa barabara hiyo ni mkakati wa Serikali ya jamhuri ya muungano wa Tanzania wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara kuu zinazounganisha Mikoa na kuunganisha Tanzania na nchi jilani na kujenga kwa kiwango cha lami barabara za mikoani.

# MATUKIO PICHANI:

## ZIARA YA RAIS SAMIA KUFUNGUA BARABARA MKOANI KIGOMA












> *Kwa mujibu wa Rais Samia, ufunguzi wa barabara hiyo iliyojengwa kwa sh. bilioni 64.7 kwa asilimia 100 ni fedha za watanzania zinazotokana na ulipaji wao wa kodi na kuwataka wafanye kazi kwa bidii.*

# KIGOMA KUWA MKOA WA KIMKAKATI




**TANROADS**
Makao Makuu Ghorofa ya 3, 10
Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue
S.L.P 11364 Dar es Salaam
Baruapepe: Tanroadshq@tanroads.go.tz

***" Miundombinu bora ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege kwa maendeleo ya Taifa"***